

# Huduma za Usaidizi wa Lugha

**Kauli mbiu:** TAHADHARI: Ikiwa unaongea Kiingereza, huduma za usaidizi wa lugha, zinapatikana kwako, bure bila malipo. Piga simu 1-800-472-2622 (Kupitia ND TTY 1-800-366-6888).

**Notisi ya Kutobagua:** Idara ya Huduma za Kibinadamu ya North Dakota inafuata sheria husika za haki za kiraia za shirikisho na jimbo na haibagui kwa msingi wa taifa, rangi, jinsia, umri, ulemavu, asili ya kiinchi, dini, imani za kisiasa, au hadhi kulingana na ndoa au usaidizi wa umma. Idara ya Huduma za Kibinadamu ya North Dakota haitengi watu au kuwachukulia kitofauti kwa ajili ya taifa, rangi, jinsia, umri, ulemavu, asili ya kiinchi, dini, imani za kisiasa, au hadhi kulingana na ndoa au usaidizi wa umma.

Idara ya Huduma za Kibinadamu ya North Dakota:

- Inatoa visaidizi na huduma za bure kwa watu wenye pungufu za kuwasiliana inavyofaa na sisi, kama vile:
  - Wakalimani wa lugha ya ishara wenye ujuzi
  - Maelezo yaliyoandikwa yenye miundo mengine (chapa kubwa, sauti, miundo elektroniki yanayofikika, miundo mengine)
- Inatoa huduma za lugha za bure kwa watu ambao lugha yao asili si Kiingereza, kama vile:
  - Wakalimani na wafasiri wenye ujuzi
  - Maelezo yaliyoandikwa kwa lugha nyinginezo

Ikiwa unahitaji huduma hizi, wasiliana na Idara ya Huduma za Kibinadamu ya North Dakota.

Ikiwa unaamini kuwa Idara ya Huduma za Kibinadamu ya North Dakota imeshindwa kutoa huduma hizi au imebagua kwa njia nyingine kwa msingi wa taifa, rangi, jinsia, umri, ulemavu, asili ya kiinchi, dini, imani za kisiasa, au hadhi kulingana na ndoa au usaidizi wa umma, unaweza kufaili lalamishi la haki za kiraia na: Civil Rights Officer, North Dakota Department of Human Services, Legal Advisory Unit, 600 E. Boulevard Ave., Dept. 325, Bismarck, ND 58505-0250, bila-malipo: 1-800-472-2622, Kupitia ND TTY: 1-800-366-6888, Faksi: 701-328-2173, baruapepe: [dhs1au@nd.gov](mailto:dhs1au@nd.gov). Unaweza kufaili lalamishi la haki za kiraia kibinafsi au kwa barua, faksi, au baruapepe. Ikiwa unahitaji usaidizi kufaili lalamishi la haki za kiraia, Afisa' wa Haki za Kiraia wa Idara anapatikana kukusaidia. Fomu za malalamishi zinapatikana mtandaoni kwenye <https://apps.nd.gov/itd/recmgmt/rm/stFrm/eforms/Doc/sfn00143.pdf>

Pia unaweza kufaili lalamishi la haki za kiraia na Idara ya Marekani ya Huduma za Kiafya na Kibinadamu, Ofisi ya Haki za Kiraia, kielektroniki kupitia tovuti ya ofisi ya malalamishi ya Haki za Kiraia, inayopatikana kwenye <https://ocrportal.hhs.gov/ocr/portal/lobby.jsf>, au kwa barua au simu kwenye:

Idara ya Marekani ya Huduma za Kiafya na Kibinadamu  
200 Independence Avenue, SW  
Room 509F, HHH Building  
Washington, D.C. 20201  
1-800-368-1019, 800-537-7697 (TDD)

Fomu za malalamishi zinapatikana kwenye <http://www.hhs.gov/ocr/office/file/index.html>